# MTOTO MWENYE ADABU

## Darasa la Watoto sehemu ya 10



Mch. Denis & Devis Julius

## UTANGULIZI:

Moja ya mambo ya kiroho ambayo anapaswa afundishwe mtoto tangu akiwa mdogo, ni ADABU.

Biblia inaagiza hivyo katika Wefeso 6:4

> *Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika* ***adabu*** *na maonyo ya Bwana.*

Jamii ya leo imeharibika, kwasababu ya wazazi wengi kushindwa kuwalea Watoto wao katika Adabu, wamekuwa radhi kuwalea vema katika mambo mengine labda yahusuyo elimu zao, afya zao, lakini kwenye eneo la adabu ambalo ndio muhimu zaidi wameliweka nyuma. Hivyo imepelekea shetani kupata nafasi ya kuharibu ushuhuda wao tangu wakiwa wadogo.

Ukuaji bora wa kiroho wa mtoto, sio tu kufundishwa kuomba, na kusoma Neno na kuimba, ukuaji bora huchangiwa na adabu njema, ambayo hiyo haizuki tu yenyewe ndani ya mtoto, bali inajengwa na mzazi au mlezi kwa kumfundisha tangu akiwa mdogo.

Kupitia kitabu hiki, utajua ni maeneo gani muhimu ya kumjenga mtoto, na kumsimamia ili akue katika adabu njema. Lakini pia mtoto mwenyewe ataweza kujisimamia mwenyewe kitabia pale atakapofundishwa faida za adabu njema.

**Zingatia:** Huu ni mwendelezo wa madarasa maalumu ya Watoto kuanzia umri 0-12, ikiwa hukupata madarasa tisa (9) ya nyuma, basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo mwishoni kabisa mwa kitabu hiki, ili tukupatie bure (Whatsapp). Ikiwa pia umeguswa kuchangia kazi hii ya injili ili isonge mbele, Tutamshukuru Mungu kwa ajili yako, hivyo kwa namba hizo hizo waweza kutuma mchango wako.

Mungu akubariki.

# MTOTO MWENYE ADABU.

## Adabu ni nini

Hatua ya kwanza, kama Mwalimu, wafundishe Watoto kwanza adabu ni nini.

Adabu ni

Adabu ni tabia njema na mwenendo wa heshima unaompendeza Mungu na unaodhihirishwa kwa namna tunavyotenda na kuzungumza na wengine.

## MAENEO AMBAYO ADABU INAPASWA IONEKANE.

### 1. Kwa Wakubwa:

- **kuwasalimia**

Swali kwa Watoto;

*Mwl:* Je! Mtoto anapokutana na watu wazima, waliomzidi umri, ikiwepo kaka zake na dada zake, Pamoja na asiowajua anapaswa afanyaje?

*Watoto:* Awasalimie

*Mwl:* Je! Yesu anapendezwa na sisi tunapowaamkia watu ?

Watoto: Ndio

*Mathayo 5: 47 Tena mkiwaamkia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je! Nao hawafanyi kama hayo?*
*48 Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.*

- **Kuwatanguliza.**

Swali kwa Watoto;

*Mwl:* Je! Endapo mtu mzima amekukuta, umeketi na mahali hapo Hapana sehemu nyingine ya yeye kuketi isipokuwa tu hapo ulipoketi wewe, je! Unapaswa ufanyaje?

*Mtoto:* Nimpishe aketi,

*Mwl:* Je! Ukifanya hivyo utakuwa umeonyesha kitendo gani?

*Mtoto:* Upendo, kwasababu upendo haukosi kuwa na Adabu .

*1Wakorintho 13:4-5 Upendo..haukosi kuwa na adabu;*

## 2. Adabu kwa wadogo

Ni vema mtoto kufundishwa adabu haipaswi kuonekana tu kwa wale waliomzidi umri,au walio juu yake, bali hata kwa walio chini yake. Hivyo hapaswi kuwatukana, kuwapiga, kuwasemesha kwa nguvu, bila sababu. Kinyume chake anapaswa kuwasaidia na kuwaongoza.

## 3. Adabu kwa Wageni

Mtoto afundishwe katika maeneo yafuatayo;

- Nidhamu ya kuomba vitu

Kama Mwalimu/mlezi/mzazi, ni wajibu kumjengea mtoto sifa ya kutokuwa omba-omba kwa watu wa wageni. Mtoto anapaswa afundishwe kuwa mzito kuvitamani vitu vya wageni, au awapo ugenini kutoomba-omba vitu vya kwao.

> *1Wathesalonike 4:12 ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje, wala msiwe na haja ya kitu cho chote.*

- Nidhamu ya kuongea

Kwamfano

- kutomkatiza mgeni anapozungumza,
- asipoulizwa asiingilie mazungumzo ya watu wazima bila sababu,
- akiulizwa na mgeni atazame kwa Heshimu,na ajibu anachoulizwa,
- Kutotumia maneno ya dharau, matusi au kejeli

Swali kwa mtoto:

*Mwl: Mgeni akija nyumbani kwetu, tunapaswa kuzungumzaje naye?*
*Mtoto: Kwa heshima na upole.*

**Mwl: Je, ni vizuri kumkatiza mtu mzima anapozungumza?*
*Mtoto: Hapana.*

**Mwl: Kwa nini?*
*Mtoto: Kwa sababu ni kukosa adabu.*

## 4. Adabu katika mazungumzo yake.

Mtoto anapaswa ajifunze Kusema.

- Asante:
- Tafadhali: Kwamfano Badala ya kusema: “Nipe maji.” Anaweza kusema:“Tafadhali, naomba maji.”
- Samahani
- Kutowacheka wengine: Anapoona mwenzake ana udhaifu fulani, ameshindwa darasani, au namna anavyoongea. Adabu nzuri, humstahi mwingine. Wafundishe yaliyomkuta Hamu mtoto wa Nuhu alipomuona baba yake yupo uchi, kwa kutomfunika, ikahesabika kuwa ni kitendo cha kukosa adabu.
- Kujua wakati wa kuzungumza na wakati wa kunyamaza:

## 5. Adabu katika kula.

Wanapoketi na kula wafundishe, vitu hivi:

- Wasiparamie chakula kabla ya wenzao,
- wasitupe chakula,

- wasiongee na chakula mdomoni,
- wamshukuru yule aliyewaandalia chakula,
- wasile kilicho cha wenzao,
- wawe na desturi ya kunawa mikono kila walapo chakula, .

Hizo zote ni sifa za adabu nzuri.

## 6. Adabu unaponyimwa kitu.

Mzazi anapomnyima mtoto, kitu , je! Mwitikio wa mtoto unapaswa uweje?

Je! Ni kulia, ni kupiga kelele, je! Ni kukasirika? ni kuonyesha kiburi cha kimya-kimya?

Somo: Mtoto mwenye Adabu, hujifunza sio tu kusema asante pale anaposaidiwa kitu, bali kujifunza pia KUJIZUIA pale anaponyimwa kitu. Hili ni somo kubwa sana la kumfundisha mtoto.

## 7. Adabu ya ibadani & shuleni

Mtoto Anapaswa afundishwe;

- Kuwa mtulivu,.
- Kuwa msikivu, kutopiga kelele, wala kutembea tembea ovyo.

## 8. Adabu ninapoadhibiwa.

Mfundishe pia pale anapoadhibiwa na mzazi / mlezi / Mwalimu kwasababu ya makosa yake.

Hapaswi kumfyolea, kumjibiza kwa maneno, bali kuomba msamaha, kutii na kujirekebisha mapema.

Hili ni muhimu sana mtoto kufundishwa.

> *Mithali 1:7 7 Kumcha Bwana ni chanzo cha maarifa, Bali wapumbavu hudharau hekima na adabu.*

## 9. Adabu pale ambapo, hakuna anayekutazama.

Ni muhimu kuwafundisha Watoto, kuwa adabu sio tabia tu ya nje, bali ni zao la kumcha Bwana ambalo linaanzia moyoni, wafundishe kuwa adabu ya ki-Mungu hudhihirika zaidi pale ambao watu hawawaoni.

Kwamfano, wazazi wanapokuwa wametoka nyumbani, je! Wataendelea kuwa na heshima ya nyumbani, je! Wakati ambao Mwalimu ametoka darasani, je! Wataendelea kukuaa kimya?

## 10. Faida ya adabu

- 1.Utapendwa na Mungu: Kwasababu unaonyesha sifa ya upendo, ambayo ni adabu
- Hujenga ushuhuda mzuri: Watu wanakuamini, hata utakapofanya jambo baya, watakuwa tayari kukusaidia, na kukufanya kuwa mwakilishi mzuri wa Kristo
- 2. . Hujenga nidhamu ya ndani. Hivyo utafanikiwa hata katika mambo yako mengine.

## 11. IGIZO.

Watoto hujifunza zaidi kwa vitendo zaidi ya maneno, hiyo buni igizo, labda Watoto wawili wameketi kwenye kiti, kama vile wapo kwenye chombo cha usafiri wa uma (daladala), kisha mzee mmoja akaingia na kusimama karibu nao. Mtoto mmoja akamwambia mwenzake, yatupasa tumpishe huyu mtu mzima, mwingine anasema mimi sitaki nimechoka, lakini yule wa kwanza akamwambia Mungu anatuagiza sisi tuwe na Adabu kwa wakubwa. Mara wote wanalitambua hilo, na wanamkaribisha kiti, yule mzee Pamoja na mkubwa mwingine aliyekuwa amesimama kwa muda mrefu.

Tengeneza igizo lingine, mtoto mmoja awe kama mzazi mwingine kama mtoto wa familia, kisha mgeni anaingia nyumbani mwao. Wakati mzazi anaongea na mgeni, yule mtoto anakwenda kumwomba, mgeni pesa ya pipi, mgeni anampa. Kisha mgeni anaondoka.

Baada ya hapo waulize. Je! Yule mtoto amefanya sawa?

*Watoto :* watajibu: Hapana.

*Mwl:* Angepaswa amwombe nani?

Watoto: Mzazi

*Mwl:* Je! Mungu anaagiza hivyo?

*Watoto:* Ndio biblia inasema tuwe na mwenendo wa adabu, kwa hao walio nje, tusiwe na haja ya kitu kwao.

## 12. OMBI

**Bwana Yesu, nisaidie kutembea kwa adabu, niyatii yote niliyofundishwa na wazazi wangu na waalimu. Amen.**

## 13. ZOEZI LA WIKI

Kama Mwalimu, wape Watoto zoezi la wiki, waagize, Katikati ya wiki wayafanye yafuatayo kisha wakuletee ripoti.

- Salimia watu watatu kila siku.
- Wamsaidie mzazi bila kuambiwa.

- Mwambie mtu “asante.”
- Omba msamaha kwa mtu uliyemkosea.
- Mpishe mtu mkubwa.
- Usimjibu mtu kwa hasira.
- Fanya jambo jema bila mtu kujua.

Ikiwa kama mzazi au Mwalimu, ukamfundisha mtoto, mafunzo hayo kivitendo, mara kwa mara, kwa kurudia rudia. Fahamu kuwa kuna njia hiyo hataicha hata awapo mtu mzima, naye atawafundisha kizazi kijacho, thawabu yako itakuwa kubwa mbinguni.

Bwana akubariki.

## **MAWASILIANO /SADAKA**

HUDUMA YA NURU YA UPENDO.

Mch. Denis & Devis Julius

Tel: +255 693 036 618 / +255 789 001 312

Website: wingulamashahidi.org/

Email: info@wingulamashahidi.org